

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAJI

MAMLAKA YA UDHIBITI WA
HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI
(EWURA)



TAARIFA KWA UMMA

(Imetolewa chini ya Kifungu na 19(2) (a) cha Sheria ya EWURA, Sura ya 414)

TAARIFA inatolewa kwa umma kuwa Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), imepokea maombi ya leseni kutoka kwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Same - Mwanga (Same – Mwanga WSSA) (“Muombaji”) kwa ajili ya kutoa huduma za majisafi na usafi wa mazingira katika miji ya Same na Mwanga, pamoja na sehemu za Halmashauri za Wilaya za Same, Mwanga na Korogwe zilizopitiwa na mradi wa maji safi Same - Mwanga – Korogwe. EWURA inakaribisha maoni kutoka kwa wananchi juu ya maombi hayo. Maelezo ya Muombaji yametolewa kama ifuatavyo:-

1: Jina na Anuani:
Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Same - Mwanga (Same - Mwanga WSSA), S.L.P 71, Mwanga. Tanzania. Barua Pepe: mdsamemwanga@maji.go.tz
2: Maelezo ya Leseni:
Leseni ya kutoa huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira katika miji ya Same na Mwanga, pamoja na sehemu za Halmashauri za Wilaya za Same, Mwanga na Korogwe zilizopitiwa na mradi wa maji safi wa Same - Mwanga – Korogwe
3: Vyanzo vya Maji na Miundombinu
Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Same - Mwanga ina vyanzo vikuu vya maji vya aina mbili ambavyo ni maji ya visima na maji ya chemchemi. Same - Mwanga ina jumla ya visima saba (7) ambavyo vina uwezo wa kuzalisha maji kiasi cha mita za ujazo 5,450 kwa siku na vyanzo vingine viwili (2) vya chemchemi vyenye uwezo wa kuzalisha maji kiasi cha mita za ujazo 111 kwa siku. Miundombinu ya uzalishaji na uhifadhi maji ya muombaji inajumuisha; matenki ya maji kumi na nne (14) yenye uwezo wa kuhifadhi maji kiasi cha mita za ujazo 1,609. Muombaji pia ana mtandao wa majisafi wenye urefu wa kilomita 139.92, pamoja na vilula 65.
4: Umiliki
Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Same - Mwanga inamilikiwa kwa asilimia 100 na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mtu yeyote mwenye maoni au pingamizi dhidi ya maombi tajwa hapo juu, awasilishe kwa maandishi EWURA kwa anwani iliyotajwa hapa chini ndani ya siku ishirini na

moja (21) kuanzia siku ya kuchapishwa kwa tangazo hili. Nyaraka za maombi ya leseni zinaweza kuoneshwa kwa mtu yeyote kwa maombi maalum ya maandishi.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu

Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji
Jengo la EWURA, Kiwanja Na 3, Kitalu AD, Medeli Magharibi
S. L. P 2857, Dodoma.

Simu: +255-26 2329003-3; Nukushi: +255-26 2329005;
Namba ya Bure 0800110030;

Barua pepe: info@ewura.go.tz

Tovuti: <http://www.ewura.go.tz>